



# Yesu Alituahidi Faraja

Yesu Kristo alijua kwamba wanafunzi Wake wangehitaji faraja baada ya Yeye kufa. Kwa hiyo aliwafundisha kuhusu Roho Mtakatifu. Aliahidi kwamba Roho Mtakatifu angewafariji na kuwa pamoja nao daima. Jina moja la Roho Mtakatifu ni Mfariji. Tunapokuwa na huzuni au hofu, Roho Mtakatifu anaweza kutusaidia kukumbuka upendo wa Yesu Kristo. ●

Unaweza kusoma hadithi hii katika Yohana 14:1, 16-18, 26.

## MIMI NAWENZA KUWAFARIJI WENGINE

- Je, Unamjua nani anayehitaji faraja?  
\_\_\_\_\_
- Sali na utengeneze mpango wa kuwasaidia wao.  
\_\_\_\_\_
- Tekeleza mpango wako!  
\_\_\_\_\_



Kata na uondoe kadi hii ili ikukumbushe kuendelea kusaidia kama Yesu.



Mama yangu, baba, na mimi tulitoa blanketi kwa hospitali ya watoto. Wafanyakazi wa hospitali hiyo walisema blanketi hizo zingewasaidia watoto wasiogope tena. Ninafurahi kwamba blanketi zetu zitasaidia kuwachangamsha watoto na kuwafanya wafurahi. Ilinifanya nifurahi sana pia.

**Brooklyn D., miaka 9, Texas, Marekani**

Je, ni kwa jinsi gani wewe unajaribu kuwasaidia wengine, kama Yesu alivyofanya? Andika na utuelezee.

